Uliberali – Mamboleo Ndani ya Mkukuta

Trans: Neoliberalism in the Poverty Reduction Strategy

Opportuna Leo Kweka

Makala hii inapitia mikakati ya maendeleo inayoongoza Tanzania leo. Ingawa mikakati hii inafuatwa na nchi nyingi masikini makala imeichukulia Tanzania kama mfano na kulinganisha tulikotoka, enzi za mikakati ya kupunguza umasikini. Makala inajaribu kueleza kuwa mikakati tunayofuata sasa ya kupunguza umasikini inafuata itikadi ya uliberali – mamboleo inayosisitiza sana ukuaji wa uchumi pasipo kuangalia usawa katika ugawanyaji wa faida itokanayo na mapato haya ya uchumi.